HOTUBA YA MHESHIMWA ALI SHAMUHUNA NAIBU WAZIRI KIONGOZI WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWENYE SHEREHE ZA UFUNGUZI WA SIKU YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA , MNAZI MMOJA

DAR ES SALAAM: 16 JUNI 2009

Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi;

Mheshimiwa Dalmas O. Anyango, Mwenyekiti wa Mkutano wa Sita wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma Barani Africa;

Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma Barani Afrika;

Mawaziri Wengine;

Mheshimiwa Julia Doly Joiner, Kamishna wa Masuala ya Siasa, Kamisheni ya Umoja wa Afrika;

Waheshimiwa Wabunge mliopo;

Makatibu Wakuu;

Wawakilishi wa Nchi Mbalimbali;

Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;

Watendaji Mbalimbali wa Serikali;

Ndugu Washiriki Wote wa Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma;

Wageni waalikwa;,

Mabibi na Mabwana.

Naomba nianze hotuba yangu kwa kumshukuru Mh. Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Kamati yake ya maandalizi kwa kunipa fursa na heshima ya kuwa Mgeni katika ufunguzi wa sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ambazo mwaka huu zinafanyika hapa kwetu, Dar es Salaam, Tanzania. Nawapa pongezi nyingi waandaaji wa sherehe hizi za Siku ya Utumishi wa umma kwa kujitolea kwao na kwa bidii walioonyesha katika kukamilisha jukumu hili zito. Naelewa kwamba jitihada kubwa zimewekwa kwenye kazi hii kwa maana ya muda, raslimali na mikakati ya maandalizi. Hongereni kwa kazi nzuri mliyofanya! Kwa wageni wetu wanaoshiriki kutoka nje, nawaomba watuwie radhi pale ambapo maaandalizi haya hayatafikia matarajio yao au kwa mapungufu yoyote yatakayojitokeza!

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, sisi Watanzania tumefurahi sana kupewa heshima ya kuwa mwenyeji wa sherehe hizi za kibara ambazo madhumuni yake ni kuzikumbusha Serikali za Kiafrika kuhusu umuhimu wa Utumishi wa Umma katika kutoa huduma kwa Wananchi, na katika kuunga mkono maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii. Vile vile napenda kuushukuru Mkutano wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma wa Windhoek, Namibia mwaka 2007 kwa kuichagua Tanzania kuwa mwenyeji wa Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika mwaka huu.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, Uamuzi wa kushehekea Siku ya Utumishi wa Umma Tanzania unatokana na kutambulika na kukubalika kwa juhudi za Nchi hii katika kuboresha Utumishi wa Umma Barani Afrika. Ni matumaini yangu kwamba

Washiriki wa sherehe hizi watabadilishana mawazo na uzoefu utakaowawezesha kuboresha huduma katika Nchi zao. Kusema kweli hili ndilo lengo kuu la Maadhimisho haya.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, Napenda vile vile kutambua kuwepo kwa Mawaziri na Manaibu Waziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma kutoka Afrika. Sisi tumefurahi kwamba mmeweza kuja Tanzania kusheherekea siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika pamoja nasi, hapa Dar es Salaam. Tunapenda kuwakaribisheni Dar es Salaam, kwa upande mmoja, na kwenye shrehe hizi za kibara, kwa upande mwingine. KARIBUNI SANA TANZANIA. JISIKIENI KWAMBA MMKO NYUMBANI. Tunawapongeza kwa kuacha shughuli zenu muhimu kwa ajili ya kuja Dar es salaam kushiriki katiku tukio hili muhimu. Kushiriki kwenu katika sherehe hizi ni kielelezo cha juhidi zenu za kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi wa Afrika ili kuwapa maisha bora. Vile vile uamuzi wenu wa kuja Tanzania ni kielelezo cha urafiki na mshikamano uliopo kati ya Tanzania na Nchi zenu.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, nimefahamishwa kwamba Kauli Mbiu ya Siku ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2009 ni: ***‘’kuimarisha ushirikiano thabiti baina ya serikali na wadau katika utoaji huduma na kuleta maendeleo endelevu Afrika’’***. Kauli Mbiu hiyo, ambayo itakuwa nguzo ya Mkutano wa Saba wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma Barani Afrika, unatokana na ukweli kwamba huduma nzuri zinategema kuwepo kwa ushirikiano baina ya wadu mbali mbali. Ni vema tukakubali kwamba Kauli Mbiu hiyo ni muafaka, na imeatolewa kwa wakati muafaka. Kuna mambo matatu yanayo dhihirisha umuhimu wa Kali

Mbiu hiyo. Awali ya yote Nchi nyingi za Afrika ziko katika mapambano ya kuwatoa wananchi wao katika makucha ya umasikini wa kupindukia. Ijapokuwa uchumi wa Nchi nyingi za Afrika umekuwa ukikua pole pole, Nchi hizo ziko nyuma katika kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia (Millenium Development Goals). Kwa vile Serikali pekee hazina uwezo wa kutoa huduma kwa viwango vya kuridhisha lazima hatua zichukuliwe ili kuvishirikisha vyombo na Asasi zisizo za kiserikali katika kutoa huduma kwa Wananchi.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni waalikwa, umuhimu wa Kauli Mbiu hiyo unatokana na ukweli kwamba Mategemeo ya Wananchi kuhusu huduma bora na zinazoendana na thamani ya huduma hizo (Value for money) yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kubwa. Kutoka na hali hii Wananchi Barani Afrika wamekuwa wakizibana serikali zao ili ziongeze ubora na kasi ya utoaji huduma.

Hii inatokana na kukua kwa uelewa mkubwa wa Wananchi kuhusu haki zao kunakoimarishwa na kukua kwa msukumo wa kijamii na vyombo vya habari. Pamoja na kutakiwa kuongeza ubora wa huduma, sekta ya utumishi wa umma ina changamopto ya upungufu wa bajeti ambayo haiwezi kuongezwa kwa kutegemea vyanzo vya kodi. Hali hii inaweka shinikizo katika majukumu yetu ya kila siku kama watumishi wa umma ambao wanatakiwa kuboresha huduma kwa umma kwa kutumia raslimali finyu zilizopo. Kutokana na hali hii ushirikiano baina ya wadau mbali mbali unatakiwa ili kuimarisha utoaji wa huduma.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, tokea Nchi za kiafrika zipate uhuru kumekuwepo na mabadiliko katika dunia na katika Nchi za Kiafrika. Kwa mfano, tumeona kujitokeza kwa mifumo ambayo ina uratibu wa karibu sana wa shughuli zake na mingine ambayo ina uhuru mkubwa wa maamuzi katika nchi zetu. Mienendo ya kimataifa katika maeneo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii imebadili kwa kiwango kikubwa hali iliyokuwepo miaka iliyopita kwa upande wa utoaji huduma kwa umma. Kwa upande mwingine hali hii inahitaji mbinu na mikakati mipya ya utoaji wa huduma kw aumma na uendeshaji wa uchumi wan chi zetu. Hali hii pia imekuza kwa kiwango kikubwa matarajio ya watu wetu.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yamebadilisha mbinu au njia za kuhudumia Wanchi. Kwa mfano hivi sasa Nchi nyingi zinaiga aina mpya za mifumo ya menejimenti katika utumishi wa umma (New Public Management) kutoka kwenye Sekta binafsi, ikiwemo mifumo ya mpango mkakati na mifumo mingine ya utendaji wa kimenejimenti katika kuendesha shughuli za serikali. Ni kweli kawamba matumizi ya teknolojia na mifumo mizuri ya utendaji wa kimenejimenti inaweza kuyasaidia matawi matatu ya Serikali kuboresha mazingira ya kusukuma mbele maendeleo ya Wananchi, na kuhakikisha kwamba kuna utawala mzuri, amani na utuli katika Nchi. Aidha matumizi ya teknolojia na mifumo mizuri ya utendaji wa kimenejimenti inaweza kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi. Kwa mfano uanzishwaji na upanuzi wa mifumo ya ‘’Serikali Mtandao’’ na ‘’Utawala Mtandao’’ kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) utaweza

kuviunganisha vyombo vya utumishi wa umma kwa upande mmoja, na Wananchi wa nchi zetu, kwa upande mwingine.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, Ushirikiano kati ya Serikali za Bara la Afrika na Asasi zisizo za kiserikali utasaidia sana katika kutumia teknologia na mifumo mizuri ya utendaji wa kimenejimenti ili kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, katika Afrika na Ulimwenugi kote dhana ya ushirikiano kati ya Serikali na Asasi zisizo za kiserikali siyo tena chaguo kati dhana nyingine, bali ni njia pekee ya kuboresha utawala na maendeleo ya kiuchumi. Kwa Afrika Changamoto za ushirikiano ni pamoja na kuchagua aina na mbinu za ushirikiano ambao utahakikisha kwamba rasilmali za nchi zinatumika na kuleta maendeleo endelevu kwa Wananchi, na kuhakikisha kwamba washirika katika shughuli za kutoa huduma wananufaika sawia. Ili ushirikiano uwe na maana na wa tija ni lazima washirika wakubaliwe na kushirikiswa tokea mwanzo mpaka mwisho wa mzunguko wa utayarishaji na utekelezaji wa sera za Nchi. Ushirikiano wa namna hiyo ni kwa washirika kuwa na sauti katika hatua ya maandalizi ya sera; kuwa na sauti wakati wa hatua ya kuandaa sheria; na washirika kuweza kufuatilia upatikanaji wa rasilimali, ugawaji wa hiyo rasilimali, na utekelezaji wa miradi ya huduma. Washirika muhimu katika kuleta maendele endelevu ni pamoja na vyombo vya serikali, na hasa matawi matatu ya serikali (Utawala, Bunge na Mahakama), mashirika ya Sekta Binafsi na Asasi zisizo za kiserikali.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa**,** nadhani mnafahamu kwamba Tanzania imekuwa ikisherehekea Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika kupitia maonyesho ya wiki moja juu ya kazi mbali mbali za serikali tokea mwaka 2003. Tokea mwaka huo mango mengi yamefanywa katika kuboresha maonyesho ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ili yawe chachu ya kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma. Kwa kutumia kampeni kubwa, kutoa elimu na kupata mrejesho kutoka kwa wadau mbalimbali, maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yamejenga uelewa na uwazi kuhusu huduma ambazo vyombo vya Utumishi wa Umma hutoa na kupata mrejesho kutoka kwa Wananchi kuhusu njia bora za kuboresha huduma za umma. Hizi njia mbili za mawasiliano zimeisaidia Serikali kuboresha huduma zake kwa Wananchi.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa, nimeambiwa kwamba mwaka huu, Siku ya Utumishi wa Umma Afrika imeandaliwa katika mantiki nilyoelezea hapo hivi punde. Namna hii ya maandalizi, ambayo yanajikita katika kuibua mbinu mpya za kuimarisha utendaji kupitia mrejesho kutoka kwa wadau, yatasaidia Serikali zetu kutatua matatizo yanayowakabili Wananchi wetu katika kupokea huduma na kuweka misingi endelevu ya kuboresha utumishi wa umma. Ni katika msingi huu ambapo ninawashauri washiriki wote wa maonyesho kuendelea kushiriki maonesho haya na kuendelea kuongeza ubunifu zaidi katika maonesho ili yaweze kuendelea kuimarisha huduma ambazo Serikali inazitoa kwa Wananchi.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa ninavyomalizia hotuba yangu ya ufunguzi wa sherehe za maonesho ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, niruhusuni tena kwa mara nyingine kurudia changamoto ambazo zinatukabili sisi kama Serikali kama ifuatavyo:

(i) Tunahitaji kujiuliza kwamba tuko wapi katika kuwa na mpango endelevu wa kuboresha huduma. Nimetumia neno 'endelevu' kwa makusudi nikiwa namaanisha kwamba utoaji wa huduma ni mchakato unaohitaji kuimarishwa kila mara kuendana na mabadiliko yanayoendelea mahali pengine duniani. Tufanye hili tukiwa tunajua kwamba kila wakati kuna changamoto, masuala na mahitaji mapya yanayohitaji mabadiliko endelevu;

(ii) Ili kuweza kukidhi hili la kwanza utumishi wa umma unatarajiwa kushughulikia mahitaji ya umma ambayo ni muhimu kwao kwa wadau wa Serikali. Pia utumishi wa umma unatarajiwa kuwa wa kiwango cha hali ya juu cha maadili; utumishi usiotegemea upande wowote kisiasa; na utumishi unaojali sifa na uzoefu wa waajiriwa. Utumishi wa namna hi ndio utaweza kutoa huduma nzuri kwa Wananchi;

(iii) Pia tunahitaji kutekeleza majukumu yetu kimkakati zaidi kwa kuzingatia uwezo wa kile ambacho Serikali inaweza kutekeleza, kulingana na raslimali zinazopatikana na kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi. Lazima kuwepo

na uwiano mzuri wa haya yote niliyoyataja kwa sababu kukosekana kwa mojawapo kutaleta huduma hafifu na hivyo kuongeza malalamiko kutoka kwa wananchi wetu;

(iv) Pia tunahitaji kuwashirikisha wananchi wetu katika mipango oote mahsusi ya kuboresha utumishi wa umma. Tufanye hivyo tukiwa tunajua kwamba wananchi ndio wanaoilpa kodi inayohimili utoaji wa huduma za umma, na pia wao ndio wapokeai wa huduma tunazowapatia kwa kutumia kodi zao; na

(v) Mwisho ni lazima tufikirie kuhusu utoaji huduma bora na si bora huduma. Suala hili ni muhimu kwa sababu litasaidia kujenga imani kwa watu wetu, imani ambayo itawafanya wananchi kuwa tayari kulipia huduma za umma kupitia kodi na kwa njia nyingine za kujitolea.

Waheshimiwa Mawaziri na Wageni Waalikwa kwa sasa niruhusuni nimalizie hotuba yangu ili mpate muda zaidi wa kupanga kazi kubwa iliyoko mbele yenu. Kwa maneno hayo machache, Natamka Rasmi kwamba Sherehe za Maonesho ya Kibara ya Siku ya Utumishi wa Umma Afrika yamefunguliwa rasmi

Nawashukuru Sana Kwa Kunisikiliza na Nawatakieni Maonesho Mema!